**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO**

**SINGIDA VTC**

**2025**

Simu: +(255) 26 2502281

Nukushi:+(255) 26 2502931

P.O BOX 733,
Singida,
Tanzania

singidavtc@veta.go.tz
www.veta.go.tz

Kumb. Na: Tarehe:

---

Ndugu…………………………………………………………..

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA SINGIDA VTC MWAKA 2025**

MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika Fani ya ________________________ngazi ya I mwaka wa 2025 Boarding/Day
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili - mitatu (2-3)
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 13/01/2025
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni
9. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii
10. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa.
11. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo

ALPHONCINA J MSHANA
MKUU WA CHUO

Mkuu wa Chuo
VETA SINGIDA VTC
P.O. Box 733
SINGIDA

## 1: MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

Unatakiwa kuja na vitu vifuatavyo chuoni:-

| # | MAHITAJI | FANI |
|---|---|---|
| 1. | Mashati mawili meupe (mikono mifupi) ya tetroni. | **WOTE** |
| 2. | Jozi moja (1) ya viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kambavilivyo na visigino vifupi | **WOTE** |
| 3. | Jozi moja (1) ya viatu vya usalama vya karakana (safety boots) | **EL,WF,SE,SCA,PPF,MB,MVM,DSCT, CJ** |
| 4. | Vifaa vya hesabu (Mathematical Set). | **WOTE** |
| 5. | Daftari kubwa kumi (10). | **WOTE** |
| 6. | Nguo za michezo yaani T/shirt,bukta ya rangi ya blue na raba nyeusi | **WOTE** |
| 7. | Rimu moja (1) ya karatasi A4 aina ya **NOPA** au **Mondi rotatrim** kwa kila muhula wa mafunzo | **WOTE** |
| 8. | Ndoo moja (1) ya plastiki ya lita 10 | **WOTE** |
| 9. | Fagio moja (1) ya mkono mrefu ya chelewa (street bloom) | **EL,PPF, MVM** |
| 10 | Kwanja moja (1) la kufyekea | **DSCT, SE, SCA** |
| 11 | Jembe moja (1) na mpini | **CJ,AH** |
| 12 | Reki ya mkono wa chuma | **MB, WF** |

**FANI KWA KIREFU**

1. **WF-** UCHOMELEAJI NA UUNGAJI VYUMA (Welding and metal fabrication).
2. **SE-** UMEME WA MFUMO WA JUA (Solar Energy)
3. **EL-** UMEME WA MAJUMBANI (Electrical Installation).
4. **SCA-** UHAZILI (Secretarial and Computer Application).
5. **MVM-** UFUNDI WA MAGARI (Motor Vehicle Mechanics**).**
6. **PPF-** UFUNDI BOMBA (Plumbing and Pipe fitting).
7. **MB**- UASHI (Masonry and Brick laying).
8. **DSCT**- UBUNIFU WA MAVAZI (Design and Sewing Cloth Technology).
9. **CJ-**UFUNDI SEREMALA(carpentry and joinery).
10. **AH-**UFUGAJI BORA WA WANYAMA(animal husbandry)

## 2. UTARATIBU WA MALIPO MBALIMBALI

**A: MUHULA WA KWANZA**

### I. KWA FANI ZA **EL,WF,SE,SCA,PPF,MB,MVM,DSCT,CJ**

| Namba | Mahitaji | Gharama | Idadi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Ada ya Mafunzo | 30,000 | 1 | 30,000 |
| **2** | Ada ya Bweni | 30,000 | 1 | 30,000 |
| **3** | Bima ya Afya | 50,400 | 1 | 50,400 |
| **4** | Michezo | 10,000 | 1 | 10,000 |
| **5** | Tahadhari | 20,000 | 1 | 20,000 |
| **6** | Suruali | 20,000 | 2 | 40,000 |
| **7** | Overall | 30,000 | 1 | 30,000 |
| **8** | Sweta | 20,000 | 1 | 20,000 |
| **9** | Nembo | 2,500 | 2 | 5,000 |
| **10** | Kitambulisho | 5,000 | 1 | 5,000 |
| **11** | T/shirt ya Unifomu | 18,000 | 1 | 18,000 |
| JUMLA KUU KWA MWANAFUNZI WA BWENI | | | | **258,400** |
| JUMLA KUU KWA MWANAFUNZI WA KUTWA | | | | **228,400** |

### II. KWA FANI YA **AH**

| Namba | Mahitaji | Gharama | Idadi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **12** | Overcoat | 30,000 | 1 | 30,000 |
| JUMLA KUU KWA MWANAFUNZI WA BWENI WA AH | | | | **288,400** |
| JUMLA KUU KWA MWANAFUNZI WA KUTWA WA AH | | | | **258,400** |

**B: MUHULA WA PILI**

***KWA WANAFUNZI WOTE**

| Namba | Mahitaji | Bei | Idadi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya Mafunzo | 30,000/= | 1 | 30,000/= |
| 2 | Ada ya Bweni | 30,000/= | 1 | 30,000/= |
| 3 | Mahafali | 20,000/= | 1 | 20,000/= |
| 4 | Ada ya Mtihani | 30,000/= | 1 | 30,000/= |
| | | | | |
| **JUMLA KUU KWA MWANAFUNZI WA BWENI** | | | | **110,000/=** |
| **JUMLA KUU KWA MWANAFUNZI WA KUTWA** | | | | **80,000/=** |

**MUHIMU**

1. Fedha zote zitalipwa kwenye **“Control Number”** atakayopewa mwanafunzi baada ya kuripoti chuoni.
2. Wanafunzi wa Bweni wanatakiwa kufika na Godoro lenye ukubwa wa (3*4*6) lenye kava,mto wa kulalia, shuka mbili (2)(rangi ya pinki kwa wasichana na bluu kwa wavulana), blanketi, chandarua, bakuli, sahani,kikombe,kijiko,ndoo au beseni la kuogea pamoja na vifaa vya usafi binafsi.
3. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu.
4. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua hii.
5. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya tarehe **13/01/2025**
6. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti ***wiki mbili*** baada ya tarehe yakufungua chuo.
7. Wanafunzi walio na umri wa miaka 18 na kuendelea waje na namba zao za NIDA zitatumika katika mchakato wa Bima ya afya.
8. Wanafunzi wote waje na nakala za vyeti vyao vya darasa la saba na au kidatocha nne
9. Wanafunzi wote watavaa soksi nyeupe kama sare ya chuo.

Mkuu wa Chuo
VETA SINGIDA VTC
P.O. Box 733
SINGIDA

**MKUU WA CHUO**
**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - SINGIDA**

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:**

### 1. MAHUDHURIO:

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:20 asubuhi.Hii ina maana ifikapo saa 1:20 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni, ADHABU KALI ITATOLEWA KWA WACHELEWAJI.

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali Au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na Mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa.

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.

(d) Mahudhurio ya mafunzo yaliyo chini ya 85% yatasababisha mwanafunzi kutoruhusiwa kufanaya mitihani yake ya mwisho.

### 2. MAVAZI:

(a) Sare ya chuo ni suruali ya bluu na shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

(b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

### 3. USAFI WA MWILI:

(a) Hairuhusiwi kuvaa heleni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo. Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

**(b) NYWELE KWA WAVULANA:**

i Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hairuhusiwi kabisa.

ii Ndevu haziruhusiwi,Ndevu za aina zote haziruhusiwi mustachi/sharubu.

**(c) NYWELE KWA WASICHANA:**

(i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma.

**(ii) Kucha zisifugwe kabisa wala kupaka rangi.**

### 4. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:

(a) Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuoau mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja.

(b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.

(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. **UGOMVI:**

Ugomvi kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.ULEVI: Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

6. **ULEVI**

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo anavuta sigara,bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa Chuo mara moja

7. **MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bilaya kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

9. **LUGHA:**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.

10. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

11. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi.

**ONGEZEKO LA SHERIA KWA WANACHUO WA BWENI**

12. Hairuhusiwi kutoka nje ya Chuo wakati wowote bila kibali maalum, Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:

    (i) Jumapili tangu saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni
    (ii) Jumamosi tangu saa 7:30 mchana hadi saa 12 jioni

13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha langu kuu na sare ya Chuo. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang’anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni.

14. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kibali atasimamishwa masomo.

15. Hairuhusiwi kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16 (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.

(b) Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa Chuo bila ruhusa au kibali.

17 Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.

18 Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 za usiku.

19. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo, ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

- Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.
- Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

20. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

21. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya Chuo itatolewa na Ofisi ya Mkuu wa Chuo.

**22. Ruhusa ya kutoka Chuoni Jumamosi saa 7:30 mchana hadi saa 12:00 jioni. Jumapili na siku za sikukuu saa 12 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mhusika aweke muda wa kutoka na kusaini arudipo.**

**MKUU WA CHUO**
**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI – SINGIDA**

Mkuu wa Chuo
VETA SINGIDA VTC
P.O. Box 733
SINGIDA

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY (VETA) SINGIDA
VOCATIONAL TRAINING CENTRE

**THE MEDICAL OFFICER**

…………………………………

…………………………………

…………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine the above named candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as/an

(i) Eyesight …………………………..

(ii) Hearing …………………………..

(iii) Asthma ……………………………

(iv) Other serious disease ………

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/ until for training as above.

Date **………………** Designation **………………** Signature & official Stamp **……….**

**MKUU WA CHUO**
**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - SINGIDA**

Mkuu wa Chuo
VETA SINGIDA VTC
P.O. Box 733
SINGIDA

# FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi ....................................................................ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani

niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo.

Sahihi ..........................................　　　　Tarehe ..............................

**b) MDHAMINI**

Mimi .................................................. Mahusiano……………………………

S. L. P. …………………………… SIMU ……………………………..

Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (Ada) pamoja na nauli wakati wote wa kwenda na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo ya awali.

Sahihi ..........................................　　　　Tarehe ..............................

**MKUU WA CHUO**
**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI – SINGIDA**

Mkuu wa Chuo
VETA SINGIDA VTC
P.O. Box 733
SINGIDA